UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Hizb ut Tahrir/ Kenya Yafanya maandamano baridi kutoa mwito wa Hatua ya Kijeshi dhidi Umbo la Kiyahudi

**HABARI NA MAONI**
Mpango wa Sykes-Picot wa kugawanya nchi unatumbukiza Afrika kwenye Ghasia na Machafuko Zaidi

**MATOLEO**
Enyi Majeshi:
[ما لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ]

**MATOLEO**
Uhamisho au Ukombozi, enyi Umma wa Kiislamu?



**Afisi ya Habari Kenya**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 08/1446 Ijumaa,20 Shawwal 1446 H 18/04/2025 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Hizb ut Tahrir/ Kenya Yafanya maandamano baridi kutoa mwito wa Hatua ya Kijeshi dhidi Umbo la Kiyahudi




Kufuatia mauaji ya halaiki yanayoendelea kufanywa na umbo la Kiyahudi dhidi ya watu wa Gaza, Hizb ut Tahrir/ Kenya siku ya Ijumaa tarehe 18 Aprili, ilifanya maandamano baridi baada ya Swala ya Jumaa katika miji ya Mombasa na Nairobi. Katika Jiji la Pwani, maandamano haya yalifanyika nje ya Masjid Nur, huku Nairobi yakafanyika katika Masjid Hidaya mtaani Eastleagh. Malengo makuu kwenye maandamano hayo ilikua ni kutoa mwito kwa Majeshi katika nchi za Kiislamu kuvunja minyororo ambayo watawala wao wamewaweka katika ngome zao ili mara moja waende kuukomboa watu wa Gaza na Al-Aqsa kutoka katika makucha ya Mayahudi walioukalia kwa mabavu.

Maandamano hayo baridi yalimalizika kwa kufanya mkutano mfupi na waandishi wa habari juu ya mashambulizi yanayoendelea dhidi ya watu wa Gaza na Filastin ardhi iliobarikiwa. Katika majumuisho hayo, Shabani Mwalimu (Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya), Ustadh Mahad Ali -Mwenyekiti wa CCC pamoja na Ali omar Mjumbe wa Ofisi ya Vyombo vya Habari walikariri kuwa serikali pekee inayoweza kuhamasisha jeshi la Waislamu dhidi ya jeshi la Jumuiya ya Kiyahudi ni Dola ya Khilafah (Ukhalifa) kwa njia ya Utume; ina uwezo wa kukomesha kiburi na ubakatili wa Wayahudi
Kwa ujumla Ummah ulikumbushwa juu ya kazi yao tukufu ya kurudisha mfumo wa maisha wa Kiislamu kwa kusimamisha tena dola ya Khilafah kwa njia ya Utume ambayo itayakusanya majeshi ya Kiislamu dhidi ya umbo la Wayahudi linaloungwa mkono na Magharibi.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir**
**Kenya**

# HABARI NA MAONI
# Mpango wa Sykes-Picot wa kugawanya nchi unatumbukiza Afrika kwenye Ghasia na Machafuko Zaidi

**Habari**

Kufikia Machi 30, 2025, Sudan Kusini inakabiliwa na mvutano wa kisiasa na ghasia zinazoongezeka, zinazotishia amani tete iliyoanzishwa kwenye makubaliano ya 2018. Kukamatwa kwa Makamu wa Kwanza wa Rais Riek Machar mwishoni mwa mwezi Machi kumezidisha hofu ya kurejea kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe. Kuzuiliwa kwa Machar, pamoja na washirika wake, kumepelekea chama chake kutangaza kuvunjika kwa makubaliano ya amani, kutokana na kukosekana kwa utashi na nia nzuri ya kisiasa kuelekea amani na utulivu.

**Maoni**

Inafahamika vyema kuwa Marekani ilisukuma ajenda ya utekelezwaji wa kutenganisha Sudan Kusini na kuanzishwa kwa dola ndani yake. Marekani iliunda vuguvugu la kujitenga lililoitwa Sudan People's Liberation Movement mwaka 1983, likiongozwa na wakala wake, John Garang, kufanya kazi ya kuwadhibiti waasi wote na harakati zao katika harakati moja. Zaidi ya hayo ni kweli Marekani ndiyo iliyomleta Rais wa zamani wa Sudan Omar al-Bashir madarakani mwaka 1989, na kumtaka awekeze ushawishi wake nchini humo, na kisha kutekeleza wazo la kutenganisha Kusini.

Izingatiwe kuwa Sudan Kaskazini na Kusini iligeuzwa kuwa ni eneo la ushawishi wa Marekani na Ulaya hasa Uingereza kwa sababu ya ushawishi wake katika Sudan ya zamani na mawakala wao huko, imeendelea kujaribu kuingilia kati kila inapowezekana, ili kurejesha ushawishi wake nchini Sudan, au angalau kushirikiana na Amerika, hata ushawishi mdogo huko.

Kwa muktadha huu, ushindani kati ya vibaraka wa nchi za magharibi yaani Rais Salva Kiir (a Dinka) na Makamu wa Rais wa zamani Riek Machar (a Nuer) umesababisha Sudan kusini katika machafuko. Nchi hii imegawanyika sana kwa misingi ya kikabila, hasa kati ya jamii za Dinka na Nuer. Jeshi la Wazungu la Nuer (wanamgambo wa kikabila) hivi karibuni walishambulia vikosi vya serikali huko Nasir, na kusababisha kuhama kwa watu wengi. Maazimio yote yaliyofikiwa kati ya wapinzani wawili kama vile Makubaliano ya Amani ya Addis Ababa yamekiukwa, jambo ambalo limeifanya nchi kuwa na machafuko zaidi. Ushindani huu kati ya Kier na Machar unatokana na mvutano wa kimaslahi kati ya mataifa ya kigeni ambao ni wahusika wakuu wenye maslahi nchini Sudan Kusini. Nia yao ni kupora rasilimali pamoja na mafuta.

Fikra jumla ya kugawanya nchi ni mipango ya makafiri wa kikoloni ili kusambaratisha biladi zetu. Afrika ambayo ni makao ya vuguvugu kadhaa za wanaotaka kujitenga lazima itambue kwamba kupitia kujitenga itajimaliza yenyewe kwa kujisoza kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe. Sudan Kusini inapaswa kutoa ushahidi wazi wa hatari ya njama hii ya wakoloni. Wakoloni sasa wamejiingiza katika mpango mpya wa kutenganisha Darfur. Wasomi wa Kiafrika na Ummah kwa ujumla wanapaswa kusimama kidete dhidi ya njama za madola ya kikoloni ya Magharibi, hususan Marekani, na kuwazuia wale wanasiasa ambao wamejitia kwenye nira ya mabepari na wanatekeleza njama zao dhidi ya ardhi yetu.

Ni kupitia Khilafah Rashida, kwa njia ya Utume ndio utakaoziunganisha ardhi zetu na kuziondolea ardhi zetu wakala au kibaraka yeyote aliyeshughulika na ardhi zetu. Kuleta hesabu kwa yeyote aliyeuza ardhi zetu kwa faida ya kidunia. Ni Khilafah pekee inayoweza kutuunganisha dhidi ya adui na ndipo tunaweza kutazama kuanguka kwao.


**Imeandikwa kwa Niaba ya Ofisi kuu ya Habari ya Hizb ut- Tahrir na**

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa vyombo vya habari Hizb ut-Tahrir Kenya.**

## Enyi Majeshi:

[ما لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ]

**“Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache.**



*Endelea... UK 5*

Mayahudi wameanza tena kampeni yao kali ya anga, bahari na nchi kavu dhidi ya Gaza kuanzia tarehe 18/3/2025, na hadi leo. Uvamizi wao umeenea hadi kwa watu, miti na mawe, na kuua zaidi ya wanawake 400, watoto na wazee. Hii ilikuwa baada ya takriban miezi miwili ya kile walichodai kuwa ni usitishaji vita, lakini waliuvunja. Mayahudi ni watu makhaini ambao wanazuilika tu kwa yale aliyoyataja Mwenyezi Mungu Al-Qawi Al-Aziz (Mwenye nguvu) katika aya hii:

فَإِمَّا تَثْقَفَنَّهُمْ فِي الْحَرْبِ فَشَرِّدْ بِهِمْ مَنْ خَلْفَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ

“Basi ukiwakuta vitani wakimbize walio nyuma yao ili wapate kukumbuka.” [Al-Anfal: 57].

Hakuna kitakachowazuia isipokuwa "Khandaq (Vita vya Handaki)" mpya inayoondoa mizizi yao, na Khaybar anayorudisha kuwapiga kama ilivyowapiga Thamud. Vyenginevyo, wamezoea kuvunja maagano, na hawa hapa wanafanya hivyo.

[‘Israel’ ilianzisha tena vita vyake katika maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Gaza kwa msururu wa mashambulizi makali yaliyoua mashahidi 412 na kujeruhi mamia. (Al Jazeera,18/3/2025)].

[Afisi ya Waziri Mkuu wa ‘Israel’ Benjamin Netanyahu ilitangaza, mapema Jumanne asubuhi, kwamba maeneo shahaba ya Hamas yalishambuliwa kote katika Ukanda wa Gaza. Taarifa hiyo iliongeza: "Israel, kuanzia sasa na kuendelea, itachukua hatua dhidi ya Hamas kwa kuongeza nguvu za kijeshi." (Sky News Arabia, 18/3/2025)].

[Waziri wa Habari wa Ikulu ya White House Karoline Leavitt alisema kuwa 'Israel' ilishauriana na utawala wa Rais wa Marekani Donald Trump kuhusu uvamizi wake huko Gaza mnamo siku ya Jumanne. (Al Hurra, 18/3/2025)].

Mauaji na uvamizi wote huo wa kinyama ulifanyika mbele ya macho ya majeshi ya nchi za Waislamu hususan zile zinazoizunguka Palestina kama vile Misri, Jordan, Saudi Arabia, Uturuki na Iran, bila kusahau zile nchi zilizojishughulisha na udhalilishaji wao wenyewe, kama vile Lebanon, Iraq na Syria! Licha ya hayo yote, watawala wanaiomba Marekani na jumuiya ya kimataifa kuwatia shinikizo Mayahudi, katika wakati ambapo Marekani ndiyo inayowaunga mkono. Ama watawala wenyewe, wametosheka tu na kulaani pekee, kana kwamba kulaani huku kutaregesha uhai kwa shahidi, kuleta uponyaji kwa aliyejeruhiwa, au kukomboa hata shubiri moja ya Ukanda wa Gaza! Mwenyezi Mungu awaangamize, wamedanganyika kiasi gani.

Misri, ambayo iliwafurusha Makruseda na Watatari, inaridhika na kuwalaani kwa taarifa tupu zisizo na maana! (Wizara ya Mambo ya Nje ya Misri ililaani uvamizi wa ‘Israel’ kwenye Ukanda wa Gaza katika taarifa yake mnamo siku ya Jumanne, ikiuita kama "ukiukaji wa wazi wa makubaliano ya usitishaji vita na ongezeko la hatari ambalo linatishia matokeo mabaya kwa utulivu wa eneo hilo." Imetoa wito kwa jumuiya ya kimataifa "kuingilia mara moja ili kukomesha uvamizi wa 'Israel' kwenye eneo la ukanda wa Gaza ili kuzuia kutokea tena kwa ghasia na kupambana na ghasia." (Sky News,18/3/2025).

Na Jordan, ardhi ya Yarmouk, vita vikuu vilivyoondoa mamlaka ya Kirumi kutoka Ash-Sham, pia ililaani! (Kwa upande wake, Waziri Mkuu wa Jordan, Jaafar Hassan alisisitiza mnamo Jumanne kwamba vita vinavyoanzishwa na Israel huko Gaza "ni vita dhidi ya ubinadamu." Shirika la habari la Jordan la Petra lilimnukuu Hassan akisema wakati wa kikao cha baraza la mawaziri kilichofanyika leo: “Jumuiya nzima ya kimataifa lazima ihusike na kukomesha ukatili huu ambao umelenga watoto, wanawake na wasio na ulinzi, na leo hii unawakilishwa na njaa kwa madhumuni ya uhamishaji.” (Sky News, 18/3/2025).

Ama kuhusu Uturuki, nchi ya mkombozi aliyekomesha Himaya ya Kirumi, pia inalaani kwa maneno bila vitendo (Uturuki inalaani mashambulizi mabaya ya ‘Israel’ huko Gaza, ikizingatiwa kuwa ni “awamu mpya ya sera ya mauaji ya halaiki” inayotekelezwa na taifa la Kiebrania katika ukanda huo wa Palestina. (Sky News, 18/3/202). Vilevile, jirani yake Iran, ilisema (katika taarifa ya mnamo Jumanne, Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Esmail Baghaei alidokeza kuwa mashambulizi ya ‘Israel’ dhidi ya Gaza, alfajiri ya kuamkia leo, yalisababisha vifo vya mamia ya watu, wakiwemo wanawake na watoto... Msemaji huyo wa Iran alizingatia kwamba Marekani “inahusika moja kwa moja na mashambulizi haya.” (Anadolu Agency,18/3/2025).

Kwa upande wa Saudi Arabia, imeanza kuegemea upande wa Marekani ya Trump, ikisema anachosema, bila kupinga uungaji mkono wake kwa Mayahudi. Badala yake, haiendi zaidi ya kulaani kwa maneno, kama wenzao: (Saudi Arabia ililaani kwa maneno makali mnamo Jumanne ‘Israel’ kuzidisha mauaji ya halaiki dhidi ya Wapalestina katika Ukanda wa Gaza na mashambulizi yake ya moja kwa moja katika maeneo yenye raia bila kuzingatia hata kidogo sheria za kimataifa za kibinadamu. (Anadolu Agency,18/3/2025)).

Kwa hivyo, nchi zinazoizunguka Palestina zililaani hujuma za Kiyahudi na jinai zao zinazoendelea katika Ukanda wa Gaza! Kwa hili, bila kuhamasisha jeshi au kuinua mkuki!

Enyi Majeshi katika ardhi za Waislamu, hasa zile zinazoizunguka Palestina:

Je, kuna udhuru wowote uliobaki kwa wanaoomba msamaha? Je, kuna hoja yoyote iliyobaki kwa wanaolaani? Vipi mnaweza kuona na kusikia uvamizi na

***Endelea... UK 6***

mauaji ya Mayahudi hali mmekaa katika sehemu zenu, bila kutikisika, badala ya kuelekea katika ardhi ya Al-Ribat, Palestine Ardhi Iliyobarikiwa, ili kurudisha uvamizi wa Mayahudi na kuliondoa umbile lao? Mnawezaje kukubali kukaa ilhali mnasoma maneno ya Al-Qawi Al-Aziz,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرَضِيتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ * إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَاباً أَلِيماً وَيَسْتَبْدِلْ قَوْماً غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئاً وَاللهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache * Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.” [At-Tawbah: 38-9]?!

Je, mnawatii watawala wanaofuata nyayo za makafiri wakoloni, hatua kwa hatua na kutupilia mbali utiifu kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake nyuma ya migongo yao? Hawataki kupigana na Mayahudi, kana kwamba hawaegemei upande wowote, bali wako karibu zaidi na upande wa Mayahudi. Watawala hawa wanalinda migongo ya Mayahudi wakati wanafanya mauaji huko Palestina. Utiifu wenu kwao hautakuepusheni na aibu ya dunia hii au adhabu ya Akhera, na mutajuta, lakini mutakuwa mumechelewa.

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتُّبِعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوُا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ * وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّ لَنَا كَرَّةً فَنَتَبَرَّأَ مِنْهُمْ كَمَا تَبَرَّءُوا مِنَّا كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ

“Walio fuatwa watakapo wakataa wale walio wafuata, na hali ya kuwa wamekwisha iona adhabu; na yatakatika mafungamano yao * Na watasema wale walio fuata: Laiti tungeweza kurudi tukawakataa wao kama wanavyo tukataa sisi! Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyo waonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni.” [Al-Baqarah: 166-7].

Kuwatii watawala katika kumuasi Mwenyezi Mungu ni kosa kubwa.

يَوْمَ تُقَلَّبُ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يَا لَيْتَنَا أَطَعْنَا اللهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَا * وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلَا

“Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa katika Moto. Watasema: Laiti tungeli mt'ii Mwenyezi Mungu, na tungeli mt'ii Mtume! Na watasema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwat'ii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio walio tupoteza njia.” [Al-Ahzab: 66-67]

Enyi Majeshi... Je, hakuna miongoni mwenu mwenye hekima wa kuliongoza jeshi na kutupa ushindi wa kutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu Al-Qawi Al-Aziz?

وَعَدَ اللهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao” [An-Nur: 55]. Je, hakuna miongoni mwenu mwenye hekima atakayeliongoza jeshi na kutunusuru katika kusimamisha Khilafah baada ya utawala huu dhalimu ambao tunaishi ndani yake ili kutimiza bishara njema ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw)?

«ثُمَّ تَكُونُ مُلْكاً جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللهُ أَنْ تَكُونَ ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا، ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ ثُمَّ سَكَتَ»

“Kisha utakuwepo utawala wa kidhalimu **(ملكًا جبرية),** na utadumu kwa muda anaotaka Mwenyezi Mungu, kisha atauondoa akipenda kuuondoa. Kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume.” Kisha (saw) akanyamaza.” Je, hakuna mwenye hekima miongoni mwenu ambaye ataliongoza jeshi na kuvunja minyororo iliyotengenezwa na watawala wa Ruwaibidha (wasio na maana, wajinga) ya kutopigana na Mayahudi? Kisha askari wa Uislamu watoke na askari hawa wanali yale aliyotufahamisha Mkweli, Mwaminifu: Al-Bukhari amepokea katika Sahih yake:

« ..تُقَاتِلُكُمُ الْيَهُودُ فَتُسَلَّطُونَ عَلَيْهِمْ»

“Mayahudi watapigana nanyi, nanyi mtawashinda...” na Muslim amepokea katika Sahih yake:

« ..لَتُقَاتِلُنَّ الْيَهُودَ فَلَتَقْتُلُنَّهُمْ»

“Kwa yakini mtapigana na Mayahudi na kwa yakini mtawauwa…”

Na kisha mutaling’oa umbile la Kiyahudi kutoka katika Ardhi iliyobarikiwa, na kisha Ardhi Iliyobarikiwa itarudi kwenye Makaazi ya Uislamu (Dar ul-Islam), kama Umar alivyoifungua, Salah ud-Din akaikomboa, na Abdul Hamid akaihifadhi!

وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ

“Na siku hiyo Waumini watafurahi * Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.” [Ar-Rum: 4-5].

**H. 19 Ramadan 1446**

**M. : Jumatano, 19 Machi 2025**

**Hizb-ut-Tahrir**

# Uhamisho au Ukombozi, enyi Umma wa Kiislamu?

Dhalimu wa Marekani, Trump, alisema katika mkutano na waandishi wa habari pamoja na mhalifu Netanyahu jioni ya Jumanne, 4 Februari 2025: "Marekani itachukua Ukanda wa Gaza, na tutafanya kazi nayo pia" Aliongeza, "Tutageuza Ukanda wa Gaza ulioharibiwa kuwa Riviera ya Mashariki ya Kati." Alizungumzia juu ya umiliki wake wa muda mrefu wa Gaza na alisisitiza taarifa yake ya awali kuhusu kuwahamisha watu wa Gaza, ambapo alisisitiza kutiishwa kwa watawala wa Misri na Jordan na wasaidizi wao, akisema: "Misri na Jordan zilisema hazitapokea wakaazi kutoka Gaza, na mimi nasema lazima watapokea." Hapo ndio watawala watiifu, wasaliti.

Trump anawatishia watu wa Palestina kwa janga jipya lisilopungua la Nakba ya 1948 au Naksa ya 1967. Anazungumza kwa kiburi kana kwamba Palestina ni milki yake au mkoa wa nchi yake. Huu ndio uhalisia ambao Waislamu hivi sasa wanauona kuhusiana na kadhia ya Palestina, ambayo imeachwa mikononi mwa Marekani na mataifa ya kikafiri.

Enyi Waislamu kwa jumla na hasa watu wa Ardhi Iliyobarikiwa:

Kutenganisha kadhia ya Palestina na Uislamu na Umma wa Kiislamu, na kuiachia Marekani na Kamati ya Kimataifa, na kuifungamanisha na maazimio ya kimataifa kutasababisha tu kufutwa kwa kadhia ya Palestina. Huu ni uhalisia ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu ametutahadharisha nao, akituita kwa tahadhari.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ تُطِيعُوا الَّذِينَ كَفَرُوا يَرُدُّوكُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا خَاسِرِينَ
* بَلِ اللَّهُ مَوْلَاكُمْ وَهُوَ خَيْرُ النَّاصِرِينَ

“Enyi mlio amini! Ikiwa mtawat'ii walio kufuru watakurudisheni nyuma, na hapo mtageuka kuwa wenye kukhasiri. Bali Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wenu, naye ndiye bora wa wasaidizi.” [Surat Aal-i-Imran:149-150].

Kuikabidhi kadhia ya Palestina na Msikiti wa Al-Aqsa kwa tawala za wasaliti na Mamlaka ya Palestina kumeliwezesha umbile la Kiyahudi kuendelea, kupanua makaazi yake, na kutoa ulinzi kwa mauaji na kuhamishwa kwenu kutoka kwa ardhi yenu. Msidanganywe na kauli zao tupu za kukataa uhamishwaji; hawa ni washirika katika uhalifu. Yeyote anayekubali uharibifu atakubali uhamishwaji, na wale waliotiwa doa la khiyana na usaliti, ambao wameiacha ardhi, bila shaka watakubali kuhamishwa. Iwapo suala la Palestina halitarudishwa kwa Uislamu na Umma wa Kiislamu, na ikiwa majeshi ya Waislamu hayatahamasishwa kuzipindua tawala za vibaraka na kufanya jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu ili kuikomboa ardhi takatifu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt), Palestina na ardhi za Waislamu zitaendelea kukandamizwa na Marekani, Mayahudi na watawala wao vibaraka.

Enyi Waislamu: Kauli za Trump kuhusu Palestina, Canada, Panama, China na nyinginezo ni taswira ya kweli ya fikra za madhalimu wa kibepari. Kwao, dunia si kitu zaidi ya maslahi na faida. Hii ndiyo dhati ya mfumo wa kibepari, na nchi zote za Magharibi hufikiri kwa kuzingatia haya. Mfumo wa kibepari umejengwa juu ya utumizi na ubinafsi, wenye kuzalisha viongozi ambao ni wauaji na maadui wa wanadamu. Viongozi wa mfumo huu wamefanya mauaji ya kikabila katika koloni walizozikalia kimabavu.

Leo hii, dunia inaishi katika giza la ubepari na ukafiri na itaendelea kutangatanga katika mashimo haya ya giza hadi pale Khilafah itakapoiokoa. Kutokuwepo kwa Khilafah yenye nguvu kumepelekea vita viwili vya dunia, na kuua watu wapatao milioni 100, na mitambo yao ya kuua bado inafanya kazi kwa njia mbalimbali. Barani Afrika, zaidi ya watu milioni 20 waliokimbia makaazi yao wanateseka kwa njaa, magonjwa, na mizozo inayochochewa na dola kubwa za Magharibi. Ulimwengu leo umesimama kwenye ukingo wa vita vyenye uharibifu ambavyo vitaangamiza watu na ardhi.

Ulimwengu mzima leo hii unauhitaji sana Umma wa Muhammad (swt), kwa kuwa ndio Umma pekee wenye uwezo wa kuokoa wanadamu. Sisi tuna ujumbe wa Mola Mlezi wa walimwengu wote, unaoondoa giza na unatupunguzia ugumu wa maisha. Ni Sharia ya Uislamu, rehma ya Mwenyezi Mungu kwa walimwengu.

Enyi Majeshi katika ardhi za Waislamu, Enyi Maafisa na Makamanda:

Je! haujafika wakati wa nyoyo zenu zinyenyekee kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na yaliyo teremshwa kwa haki? Je, haujafika wakati wa nyinyi kusimama kwa heshima na kupindua viti vya watawala wanaokutiisheni nyinyi na Ummah wenu kwenye aina zote za udhalilishaji? Je, wakati haujafika kwenu kutambua kwamba Ummah wenu, Ummah wa Muhammad (swt), una uwezo wa kuokoa wanadamu?

Je, haujafika wakati wa nyinyi kutambua kwamba muna uwezo wa kuishinda Amerika, kuikomboa Bayt al-Maqdis, na kusimamisha uadilifu miongoni mwa watu?

***Endelea... UK 8***

Je, wakati haujafika wa nyinyi kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرَضِيتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ * إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَاباً أَلِيماً وَيَسْتَبْدِلْ قَوْماً غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئاً وَاللهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

"Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache. Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu." [Surat At-Tawba:38-9].

Enyi Umma wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt), enyi Umma bora ulioletwa kwa ajili ya wanadamu:

Watu wa Palestina leo hii wanakabiliwa na kifo na kuhamishwa, na nyinyi hamna budi ila kusimama kwa ajili ya ukombozi, kujikomboa kutokana na watawala madhalimu na vibaraka wa Magharibi, na kuandamana na majeshi yenu kuelekea Bayt al-Maqdis ili kuikomboa na kuitakasa kutokana na uchafu wa wavamizi. Ucheleweshaji wowote au kusitasita katika kuwapindua watawala vibaraka katika ardhi za Kiislamu kutatugharimu sana katika damu, watoto na mali zetu.

Jukumu lenu kwa wanadamu, kama mulivyolazimishwa na Uislamu, linawawajibisha kutenda kwa nguvu zenu zote ili kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume na kuziunganisha ardhi za Kiislamu ili kusimama dhidi ya Marekani na maadui wa wanadamu miongoni mwa madhalimu wa kibepari.

Imani ya kweli, kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi, na kukata mafungamano na Shetani na washirika wake, ndivyo vinatufanya tustahiki ushindi wa Mwenyezi Mungu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ تَنْصُرُوا اللهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

"Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu." [Surat Muhammad:7]. Endapo Mwenyezi Mungu atatunusuru, hakuna wa kutushinda:

[إِنْ يَنْصُرْكُمُ اللهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمْ وَإِنْ يَخْذُلْكُمْ فَمَنْ ذَا الَّذِي يَنْصُرُكُمْ مِنْ بَعْدِهِ وَعَلَى اللهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ]

"Akikunusuruni Mwenyezi Mungu hapana wa kukushindeni, na akikutupeni ni nani, basi, baada yake Yeye ataye kunusuruni? Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu." [Surat Aal-i-Imran:160]. Jihadharini na mfano wa Wamongolia; waliua mamilioni, lakini walishindwa na ikhlasi ya waumini wa Ain Jalut.

Kumtegemea kwetu Mwenyezi Mungu, Mtukufu, hakutenganishwi na imani yetu kwa Ummah wetu, ambao Mwenyezi Mungu ameukabidhi Kitabu chake na wahyi Wake. Msibabaishwe na nguvu na kiburi cha Marekani, kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu zaidi juu yao, na nguvu zake zinakunusuruni. Simameni, enyi Waumini wenye nguvu, tangazeni haki, msiogope ila Mwenyezi Mungu, wapindueni watawala vibaraka, toeni ahadi ya utiifu (bay'ah) kwa Khalifa atakayesimamisha Dini baina yenu, na Mwenyezi Mungu atatimiza ahadi yake ya kudhihirisha Dini yake.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَى وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ

"Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya Haki ipate kushinda dini zote, ijapo kuwa washirikina watachukia." [Surat At-Tawba:33].

Amesema Tamim al-Dari (ra): Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt) akisema:

«لِيَبْلُغَنَّ هَذَا الْأَمْرُ مَا بَلَغَ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ، وَلَا يَتْرُكُ اللهُ بَيْتَ مَدَرٍ وَلَا وَبَرٍ، إِلَّا أَدْخَلَهُ اللهُ هَذَا الدِّينَ يُعَزُّ عَزِيزٌ أَوْ يُذَلُّ ذَلِيلٌ، عِزّاً يُعِزُّ اللهُ بِهِ الْإِسْلَامَ وَأَهْلَهُ، وَذُلّاً يُذِلُّ اللهُ بِهِ الْكُفْرَ»

"Hakika jambo hili litafika kila mahali panapoguswa na usiku na mchana. Mwenyezi Mungu hataiacha nyumba ya udongo wala manyoa ila ataiingiza dini hii, na kuleta heshima kwa waheshimiwa na kuwafedhehesha waliofedheheka—heshima anayoipa Mwenyezi Mungu Uislamu na watu wake, na fedheha anayoifanya Mwenyezi Mungu juu ya ukafiri."

Ewe Mwenyezi Mungu, tufikishie kheri hii, na zifungue nyoyo za Waislamu kwayo, na utujaalie kutoka Kwako mamlaka yenye kunusuru. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.

**H. 7 Sha'aban 1446**

**M. : Alhamisi, 06 Februari 2025**

**Hizb-ut-Tahrir**

**Ardhi ya Baraka-Palestina**